# EFATHA

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha EFATHA. Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ruhusa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk bib-lia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

EFATHA

1.Efatha nini?.............................................

2.Matendo mema ya Efatha……………………

3.Baraka ………………………………………….. …

4.Utajiri…………………………………………………

5.Utumishi ………………………………………………

6.Kuokoka…………………………………………………

7. Mwisho…………………………………………………

# 1. EFATHA NI NINI?

Efatha maana yake **funguka** tunaipata ktk **Marko 7:32—35**

**“”Wakamletea kiziwi, naye ni mwenye utasi, wakamsihi amwekee mikono. Akamtenga na mkutano faraghani, akatia vidole vyake masikioni mwake, akatema mate, akamgusa ulimi, akatazama juu mbinguni, akaugua, akamwambia, Efatha, maana yake, Funguka. Mara masikio yake yakafunguka, kifungo cha ulimi wake kikalegea, akasema vizuri “**

Ni mojawapo ya mambo aliyotumwa Yesu na Baba yake wa mbinguni kwa waisraeli kama masihi yaliyotabiriwa na Nabii Isaya;

**Luk 4:17-19**

“ Akapewa chuo cha nabii Isaya, akakifungua chuo, akatafuta mahali palipoandikwa,

Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta

- kuwahubiri maskini habari njema.
- Amenituma kuwatangazia wafungwa **kufunguliwa** kwao, ,,,,,,,”

Ukisoma ktk maandiko ya hapo juu ktk kitabu chako cha biblia Yesu

Alitumwa na Baba wa mbinguni kwa Israeli mambo manne hata leo watumishi wake aliowatuma hutenda na kuwapa huduma Yesu huwatumia kutenda mojawapo ya hayo mambo aliyotumwa,

Huduma yeyote ya kiroho ya waliokoka ya kanisa lazime iwe jamho mojawapo alilotumwa Yesu.Iwe ni huduma ya kitume, kinabii, kiualimu,kichungaji,kiunjilisti,kimiujiza, na kiponyaji.

Kanisa waliokoka wote wanapaswa kujitoa kwa sehemu kidogo ktk kuhubiri au kushuhudia wenye dhambi waokoke ukianzia familia yako kisha rafiki au mfanyakazi mnunulie hata kitabu cha mtumishi wa mungu kanisani kwako chenye sala ya kuokoka mwishoni mmpe kama una pesa ila wakati hujazoea kumkiri yesu ndio mchanga pengine unaona haya pesa yako ni ushindi wako.

## 2.MATENDO MEMA YA MUNGU—EFATHA

Yesu alitumwa na Baba wa kufungua watu  mifano hai ktk biblia inayodhirisha Yesu aliwafungua waisraeli vifungo vya kiroho walikuwa wafungwa walifungwa na shetani ni kama;

1) Kufunguliwa bubu na kiziwi **Marko 7:32—35**

**Wakamletea kiziwi, naye ni mwenye utasi, wakamsihi amwekee mikono. Akamtenga na mkutano faraghani, akatia vidole vyake masikioni mwake, akatema mate, akamgusa ulimi, akatazama juu mbinguni, akaugua, akamwambia, Efatha, maana yake, Funguka. Mara masikio yake yakafunguka, kifungo cha ulimi wake kikalegea, akasema vizuri "**

2)Kufunguliwa mjane aliyefungwa na shetani 18.

**Luka 13:11-16"Na tazama, palikuwa na mwanamke aliyekuwa na pepo wa udhaifu muda wa miaka kumi na minane, naye amepindana, hawezi kujinyosha kabisa. Yesu alipomwona alimwita, akamwambia, Mama, umefunguliwa katika udhaifu wako. Akaweka mikono yake juu yake, naye akanyoka mara hiyo, akamtukuza Mungu. Basi mkuu wa sinagogi alikasirika kwa sababu Yesu amemponya mtu siku ya sabato, akajibu, akawaambia mkutano, Kuna siku sita zifaazo kufanya kazi, basi njoni mponywe katika siku hizo, wala si katika siku ya sabato.**

**Lakini Bwana akajibu akasema, Enyi wanafiki, kila mmoja wenu, je! Hamfungui ng'ombe wake au punda wake siku ya sabato katika zizi, aende naye kumnywesha? Na huyu mwanamke, aliye wa uzao wa Ibrahimu, ambaye Shetani amemfunga miaka kumi na minane hii, haikupasa afunguliwe kifungo hiki siku ya sabato?** "Hayo ndio matendo mema mungu alitenda kwa waisraeli waliofungwa na shetani kwa kuwafungua akimtumia masihi wake Yesu au mwanae Yesu. Ukiwa una sehemu ndogo ya neema ya Yesu kufumngua Bubu,kiziwi au watu wenye pepo wa udhaifu hata migogo imepinda,hawawezi kujinyosha ni jambo la kawaida kwa Mtumishi wa Yesu aliyetumwa kwa hilo. Kumbuka wako wenye vibiongo na wenye pepo wa udhaifu.

## 3. BARAKA

Baraka ni mafanikio unayopato ktk wokovu wako kumtolea mungu sehemu ya ujira/mapato yako ya kazi mikono yako ijapokuwa zipo zingine si kwa matoleo.

Mfano wa Baraka mtoto,chakula na afya,kipato kuongezeka(mf;- pesa).

Ukweli wa Baraka huendana na upako wa kinabii(Mungu wa Manabii) sehemu kubwa Baraka ktk biblia inazungumzwa  na manabii.

**Jinsi ya kupata baraka**

1) Zaka / Fungu la kumi  **(Malaki  10 )**

“Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni **baraka,** hata isiwepo nafasi ya kutosha,”

2) Kutii Maagizo ya mungu **(Kumbuk 28)**

3)Ndoa  **(Mwanzo 1 : 28)**

“Mungu **akawabarikia**, Mungu akawaambia, **Zaeni, mkaongezeke,** mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi.

4)Kuombea waliokoka yaani kanisa au wenzako wabarikiwe.au kuwabariki waliokoka kwa maneno ya kinywa chako.

**Mwanzo 12:2—3**  nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe **baraka;** nami **nitawabariki wakubarikio,** naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa. Kwa waefatha kutii kufuata njia hizo nne ni za lazima ukitaka baraka za mungu wa efatha.

## 4. UTAJIRI/UKWASI

Ni kuwa na mali nyingi.Maana ni kuwa kitu cha thamani ktk wingi mfano nyumba,kiwanda,hoteli,viwanja kampuni au vitu ktk wingi mfano nyumba 70,hoteli 30,kampuni 7 na viwanda 3.

Njia ya kupata utajiri kutoka mungu

=>Kuomba **1wafalme 3: 11 — 13**

"Mungu akamwambia, Kwa kuwa umeomba neno hili, wala hukujitakia maisha ya siku nyingi; wala hukutaka **utajiri** kwa nafsi yako; wala hukutaka roho za adui zako; bali umejitakia akili za kujua kuhukumu;

basi, tazama, nimefanya kama ulivyosema. Tazama, nimekupa moyo wa hekima na wa akili; hata kabla yako hapakuwa na mtu kama wewe, wala baada yako hatainuka mtu kama wewe. Na mambo yale usiyoyaomba nimekupa, **mali na fahari,** hata hapatakuwa na mtu katika wafalme kama wewe, siku zako zote. "

Yesu anasema "**Luka 11.9 Nami nawaambia, Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa."**

Njia pekee ya kupata utajiri ni kuomba utajiri kwa Baba wa mbinguni. Mungu alimchagua sulemani hamjengee nyumba yake hakumnyima utajiri .Uombapo utajiri mtu uliyeokoka weka na nia kristo utapata na uwe mwaminifu. Mtu Uliyeokoka Mwombe Mungu utajiri wa kuchangia kazi yake mfano injili wa kanisa unapoabudu utapata ikiwa una kiu ya haki. Jibidiishe ktk kutengeneza ajira kwa wengine wekeza mfano mgahawa,- hoteli,kampuni.

Kwa waefatha mwombe mungu akupe utajiri wa efatha sehemu yako kwa ajili ya kuchangia injili. Ya efatha na kazi za mungu.wa efatha.

## 4. UTUMISHI

Ukitaka kufahamu utumishi na kusudi ulililoitiwa wewe binafsi funga na umuulize mungu ili akufunulie na uunganishe na lile la kanisa la efatha na mzaliwa wa efatha kwa wale walimaliza na kupata cheti cha efatha. Mfuate Yesu funga siku Arobaini, Usije ukatumika na shamba lako halijalimwa.

Wakati swinging unatumika bila kustawi shauku yako ya haki kutiishwa au bila furaha.

Kwa wale ambao ni viongozi wa kanisa kama wachungaji, mitume, manabii,wainjilisti, na waalimu wa efatha usimamapo jifunze kujifungamanisha na Mtume na nabii wa kanisa la Efatha

J.E Mwingira ktk umoja upate upako wa nafasi yako. Kwa kuwa unasimama mbele ya kanisa na kulihudumia kwa kutumiwa na Yesu.

Ushuhuda wa kuishi bila kutenda dhambi uwe nao kwa kumuuliza ktk semina za viongozi Mtume na Nabii J.E Mwingira na Yesu ktk maombi yako.

Tii maagizo na mafundisho utumishi na uongozi anayowafundisha ya uongozi na utumishi uwe kielelezo na mfano kwa kanisa.

Kumbuka nguvu ya roho mtakatifu uliyoipata siku za ubatizo ktk semina za viongozi kwa kupakwa mafuta na kuwekewa mkono na ile uliyoipata kupakwa mafuta na kuwekewa mkono ulipomaliza Precious Bible college uitunze kama kuna utofauti uitafute ikishindikana kamwone Mtume na Nabii J.E,Mwingira.

Kwa wale waliopata vyeti vya utumishi Mungu baada kumaliza mafundisho ya Roho mtakatifu na karama wamezifahamu na waalimu wao au walezi wa kiroho wamezitambua baada kutumika kidogo na wale waliofunuliwa na Yesu ni mitume, manabii, wachungaji, waalimu,wainjilisti,wahubiri wakubwa na nafasi nyingine ktk kanisa ni vizuri kwenda chuo cha utumishi wa mungu cha kujifunza ili utumiwe na Yesu na ngazi ya juu zaidi.

## 5. UTUMISHI

Kwa wale ambao ni wanaefatha wanaoguswa na ujumbe wa kitabu hiki

Watii usikwepe Mungu wala kutoa udhuru wakati mwingine kwa kutojitoa wokovu wako unaona hauna ustawi mkubwa hicho ulicho wahi chuo cha utumishi cha Efatha.

Jitahadi kwenda na wakati /majira ya mungu ambao mungu anaanza nao wakati ulipobatizwa na kujazwa roho mtakatifu na kuwekewa mikono na mitume na manabii J.E Mwingira.

Ahadi ya Mungu kwa watumishi wa Mungu Wa efatha watakajitoa ili-watumiwe na Yesu na Mungu kikamilifu ni hii:

Yoh 12.26

**" Mtu akinitumikia, na anifuate; nami nilipo, ndipo na mtumishi wangu atakapokuwapo. Tena mtu akinitumikia, Baba atamheshimu."**

Yesu aliwaambia maneno wale waliotaka kumfuata kwa kumtumikia kabla ya kusuluiwa na kufufuka kisha kupaa kwenda mbinguni kwa Baba wa mbinguni ambaye ni mungu wa Israeli na kuandaa makao kwa ajili ya wale watakaomtumikia. Yaani watumishi wa Yesu.

Watumishi wa efatha mnaotumikia Yesu kwa Uaminifu mtakuwa na Bwana Yesu ktk Makao matatifu kazeni mwendo . Kwa habari ya makao matakatifu msome na kutakari kitabu cha **kweli mbingu ipo kimeandikwa na choo Nam(Efatha Bookshop)**

**Efatha rule:**

**"Akili Kichwani, Yesu Moyoni na Pesa Mfukoni"**

## 15. KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

## 16. MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa yesu uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**

Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :


**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or 0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 9332

**MWENGE— DAR-ES-SALAAM TANZANIA**



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003 kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha

Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034